

## Maelezo kwa wazazi/walezi na watoto/vijana kuhusu Utafiti wa Ungdata

Mwaka huu, Utafiti wa Ungdata utafanywa katika shule-za sekondari za kiwango cha juu katika manispaa yako. Madhumuni ni ili kupata muhtasari mzuri wa hali ya malezi ya vijana ya ndani. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba watoto na vijana wengi iwezekanavyo washiriki. Utafiti huo utafanywa wakati wa muhula wa msimu wa vuli.

### MADHUMUNI YA UTAFITI HUO

- Kuwapa watoto na vijana nafasi ya kuwaambia wanasiasa na mamlaka kuhusu jinsi kukua katika manispaa ilivyo.
- Kupata ufahamu mpya kuhusu hali ya malezi ya watoto na vijana kwa madhumuni ya kazi ya manispaa/kaunti pamoja na kikundi cha umri huu.
- Kuwezesha ulinganishi pamoja na manispaa zingine na takwimu za kitaifa na kuchangia katika utafiti.

### JE, TUNAUJIZA KUHUSU NINI KATIKA UNGDATA?

- Uhusiano na shule, marafiki na wazazi
- Wakati wa kupumzika na shughuli za kupumzika
- Matumizi ya vyombo vya habari
- Afya, ustawi na ubora wa maisha
- Uonevu
- Uvunjaji wa sheria, vurugu na matumizi ya dawa za kulevya
- Viwango vya elimu vya wazazi/walezi

### JE, UTAFITI WA UNGDATA UNAFANYWAJE?

- Saa moja ya shule imetengwa ili kukamilisha utafiti huo.
- Utafiti huo unafanywa kwa njia ya kielektroniki kwa kuingia katika ukurasa wa majibu wa Ungdata ukitumia nambari ya idhini ya wakati mmoja.
- Wanafunzi wanajibu kwa kuweka alama kwenye hati iliyo na maswali ya utafiti. Kuna chaguo la kusomewa kwa sauti maswali yaliyo kwenye dodoso. Ikiwa unatumia chaguo hii, hedifoni/vifaa vya sauti vinapaswa kutumiwa.

### KUSHIRIKI NI KWA HIARI

- Utafiti huo ni wa hiari.
- Wale ambao watajibu wanaweza kuruka maswali ambayo hawapendelei kujibu, na wana chaguo la kusitisha utafiti unapoendelea, ikiwa watapendelea kuusitisha.
- Wazazi/walezi wa vijana walio chini ya umri wa miaka 18 wanaweza kuchagua mtoto wao asishiriki kwa kuarifu mwalimu wa mtoto/shule ya mtoto.

### FARAGHA

- Majibu ya washiriki yatashughulikiwa kwa usiri. Watafiti na washauri katika mradi na kampuni inayosajili majibu ndio TU watakaofikia majibu yote.
- Hakuna yeyote ambaye amejibu ataweza kutambulika matokeo ya utafiti yatakapochapishwa.
- Data ya utafiti iliyo na data ya kibinafsi ambayo sio ya moja kwa moja itahifadhiwa salama. Mwishoni mwa mwaka, miaka mitano baada ya kukamilika kwa utafiti huo, data zote hazitatambulisha waliohusika.
- Utafiti wa Ungdata umeidhinishwa na afisa wa ulinzi wa data aliye huko OsloMet (personvernombud@oslomet.no).
- Hifadhi ya data haitakuwa na data yoyote ya kibinafsi iliyo ya moja kwa moja. Kwa hivyo, pia haitawezekana kurekebisha au kufuta data ya washiriki baada ya utafiti.
- NOVA huchakata data kulingana na idhini ya washiriki.

### UTAYARI

Huduma ya afya ya shule itakuwa na hatua za utayari baada ya utafiti kwa wanafunzi wowote ambao watazihitaji.

**NANI ANAWAJIBIKA KATIKA UNGDATA?**

Utafiti huo unafanywa na Taasisi ya Utafiti wa Jamii ya Norway (NOVA) iliyo huko OsloMet (Chuo Kikuu cha Oslo Metropolitan) na kituo cha umahiri wa dawa na pombe (KoRus), kulingana na kazi iliyotolewa na manispaa.

**JE, UNA MASWALI YOYOTE?**

Tafadhali wasiliana na shule au KoRus ya eneo lako kwa maelezo zaidi kuhusu utafiti huo.

Ikiwa ungependa kupokea toleo la dodoso kwa lugha ya Kinorwei au Kiingereza, hili linaweza kupatikana kwa kuwasiliana na KoRus.